

Una swali binafasi kuhusu Ukimwi?

Piga TAYOA kuanzia saa 9:00
alasiri mpaka 3:00 usiku

HUDUMA YA BURE

0741/0744/0747/TTCL

800 448

au Celtel **148 tu**

Je, wajua?

Hufi kwa Ukimwi kwa kufanya
kazi na walioathirika...

lakini

...unyanyapaa na ubaguzi
wa watu wanaoishi na
Ukimwi huaa!

Hebu tuongee

kuhusu

Ukimwi

mahali pa kazi

Au tembelea mtandao wa
www.aidshelpline.info

au

www.chezasalama.com

kwa Kiswahili na
Kingereza

**Hatuwezi kudiriki
kufukia vichwa vyetu
mchangani kama mbuni.**

ABCT

AIDS Business Coalition Tanzania

Mavuno House, Azikiwe Street

P.O.Box 12941, Dar es Salaam

Tel: +255 (0) 22-2125113

Mob: +255 (0) 748-617228

Fax: +255 (0) 22-2125112

Email: abct@bol.co.tz



AIDS Business Coalition Tanzania
ABCT

Supported by



Ukimwi ni sehemu ya maisha yetu na shughuli yetu

ZINDUKA!

Je, una swali kuhusu Ukimwi mahali pa kazi?

Je shirika lako limetengeneza sera ya Ukimwi mahali pa kazi?

Mashirika mengi yanachukua hatua dhidi ya ukimwi, Kwa kuzuia ubaguzi na unyayapaa dhidi ya waathirika na kuelezea hatua za kinga na jinsi ya kuwatunza wagonjwa wa ukimwi mahala pa kazi.

Je, kondom husambazwa mahali penu pa kazi?

Kondom ni nzuri sana kwa kuzuia virusi vienezavyo ukimwi. Waajilri wengi husambaza kondom kama njia mojawapo ya kuzuia maambukizi kwa wafanyakazi wao.

Je, kuna mabango ya matangazo na vipeperushi vyovyote juu ya ukimwi mahali penu pa kazi?

Mabango, vipeperushi na vijitabu vya Ukimwi hupatikana bure kutoka taasisi mbalimbali za Ukimwi au za afya ya jamii. Mashirika pia huwafunza baadhi ya wafanyakazi ambao baadaye huwa waelimisha rika wa afya juu ya ukimwi kwa wafanyakazi wa rika lao.

Je, Shirika lako linasaidia katika kupatikana Kwa Ushauri nasaha na kupima Ukimwi bure?

Huduma za bure za ushauri nasaha na kupima zawezekana ziko karibu nawe. Kwa nini huduma hizi hazitangazwi mahali pa kazi?

Je, Huduma za matibabu kwa wafanyakazi ni swala muhimu kwa mwajiri wako?

Ungojwa wa Ukimwi unaongeza garama za matibabu kwa wale walioathirika.

Je, Shirika lako linachukua tahadhari dhidi ya madhara ya Ukimwi kwa waathirika na waathiriwa?

Kuna njia nyingi za kuwasaidia waathirika wa Ukimwi na familia zao, mojawapo ni matunzo ya waathirika wakiwa majumbani mwao. Huduma kama hii ni muhimu kama itatolewa mahali pa kazi.

ABCT ni Muungano wa waajiri Tanzania ambao wamejiunga pamoja kupambana dhidi ya Ukimwi.

ABCT inafanya kazi kama kituo cha:

- Kutoa ushauri kwa waajiri
- Kujenga na kubadilishana uzoefu
- Kukusanya na kusambaza habari zote zinazohusu ukimwi mahali pa kazi.

ABCT inasaidia kuweka shinikizo

- Kushawishi Serekali
- Kutafuta washirika
- Kukuza Programme za Ukimwi mahali pa kazi



ABCT

AIDS Business Coalition Tanzania

Mavuno House, Azikiwe Street

P.O.Box 12941, Dar es Salaam

Tel: +255 (0) 22-2125113

Mob: +255 (0) 748-617228

Fax: +255 (0) 22-2125112

Email: abct@bol.co.tz

Shiriki kwenye program za Ukimwi mahala pa kazi. Italinda maslahi yako ya kazini na ya muajiri. Na utaoko maisha !